

**MUHTASARI**

- Mvua ziliendelea vizuri katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua ambapo wakulima wanaendelea na shughuli za palizi.
- Mvua zinazotarajiwa kwa kipindi cha Januari 21-31, 2018 zitasaidia ukuaji wa mazao na malisho kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua.
- Mvua za nje ya msimu wa vuli zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu wa udongo kwa ajili ya malisho na mazao yaliyopandwa kwa kuchelewa.


**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA  
KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2018**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu kidogo na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kubaki Tanzania hususan katika maeneo ya nyanda juu kusini-magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi. Hali hii ilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la bahari katika Bahari ya Hindi liliendelea kuwa chini kidogo ya wastani ambapo lilisababisha maeneo ya Pwani kuwa na vipindi kadhaa vya mvua na radi. Kwa upande mwingine kumekuepo na joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola), hali iliyosababisha kupungua kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi.

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI  
CHA JANUARI 11-20, 2018**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa iliyokuwepo katika kipindi hicho, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za juu ya wastani (zaidi ya 120% ya wastani wa mvua kwa siku kumi) kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.1. Hata hivyo, maeneo mengi ya mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Geita, Simiyu, Kigoma, Tabora, Rukwa na visiwa vya Unguja na Pemba vilipata mvua za chini ya 80% ya wastani wa mvua kwa siku kumi. Pia katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Arusha, na Pwani yalipata mvua chache za chini ya 80%. Kutoka na mwenendo wa hali ya hewa kwa kipindi hiki cha siku kumi imebainika kwamba kuna ongezeko la mvua katika maeneo yanayopata misimu miwili

ya mvua hususan maeneo ya mikoa ya Morogoro (kaskazini), , Pwani, Manyara, Arusha, Mara, Mwanza na Kagera ambapo katika maeneo hayo mvua za vuli zinakwisha mwishoni mwa mwezi wa Disemba.



**Kielelezo Na. 1:** Kiasi cha mvua (% ya wastani wa siku kumi) kwa kipindi cha Tarehe 11-20 Januari, 2018.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA  
KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2018**

Kutokana na mvua za msimu zinazoendelea kunyesha, unyevunyevu kwenye udongo uliimarika katika maeneo

mengi yanayopata mvua katika msimu mmoja, ambapo umesaidia ukuaji wa mazao. Mvua za juu ya wastani ziliathiri shughuli za palizi pamoja na uwekaji mbolea mashambani. Mvua za nje ya msimu katika maeneo yanayopata mvua za vuli zimesaidia mazao yaliyopandwa kwa kuchelewa. Pia maji na malisho kwa ajili ya mifugo viliimarika katika maeneo mengi nchini.

### HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2018

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2018

**K**atika kipindi cha siku kumi za mwisho za mwezi Januari, 2018 migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) inatarajiwa kupungua nguvu kidogo wakati migandamizo mikubwa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo. Ukanda wa mvua utaendelea kubaki Tanzania hususan katika menea ya nyanda juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi, hali hii itapelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa mvua hususan katika ukanda wa pwani ya kaskazini. Kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuwepo kwa joto la juu ya wastani na hivyo kuchangia kupungua kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi. Hata hivyo, vimbunga vinatarajiwa katika maeneo ya mashariki mwa Madagascar na kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi, kanda ya kati na pwani ya kaskazini.

### HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2018

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu), Magharibi mwa nchi (Mikoa ya**

**Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi vichache vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara) na Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja navisiwa vya Unguja na Pemba):** Maeneo hayo yanatarajiwa vipindi vya mvua katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya), Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na Kanda ya kusini (Mkoawa Ruvuma):** Vipindi kadhaa vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

### MATARAJIO NA USHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2018

**M**vua zinazotarajiwa zitaendelea kuongeza unyevunyevu wa udongo kwa ajili ya ukuaji wa mazao katika maeneo yanayopata mvua za msimu mmoja wa mvua. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi wakati wa upungufu wa maji. Mvua za nje ya msimu kwa maeneo ambayo yanapata misimu miwili ya mvua zitanufaisha mazao yaliyopandwa kwa kuchelewa, japokuwa shughuli za uvunaji na ukaushaji wa mazao yaliyokomaa kama vile maharagwe zinaweza kuathirika. Mvua hizi pia zinatarajia kuimarisha ustawi wa malisho ya mifugo na upatikanaji wa maji katika maeneo mengi nchini. Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

### HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2018

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka katika mabonde ya Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu na Ruvuma kutokana na mvua zinazoendelea. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa matumizi endelevu.

Jarida lilitayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Barua pepe: (1) [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz) (2) [agromet1\\_tz@meteo.go.tz](mailto:agromet1_tz@meteo.go.tz)